**JAMHURI YA MUUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

**SHULE YA SEKONDARI NGANZA**

**FOMU YA KUJIUNGA NA MASOMO YA KIDATO CHA TANO ...............**

**MAWASILIANO**

**MKUU WA SHULE: 0784871921**
**MAKAMU MKUU WA SHULE(ME): 0755250071**
**MAKAMU MKUU WA SHULE(KE): 0755421174**
**NESI WA SHULE (KWA MAMBO YA AFYA TU): 0753967022**

**SHULE YA SEKONDARI NGANZA,**
**S.L.P 1252,**
**MWANZA**
**TAREHE ................................**

**MZAZI/MLEZI WA MWANAFUNZI .................**

**...........................................................................**

**S.L.P ........................................................................**

**YAH: MAELEZO YA KUJIUNGA KIDATO CHA TANO SHULE YA SEKONDARI NGANZA MWAKA ............................**

Ninafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na Kidato cha Tano katika Shule hii mwaka ................................ tahasusi ya ........................ Shule ya Sekondari Nganza ipo umbali wa Kilometa 12 kusini mashariki mwa mji wa Mwanza.

## 1. USAFIRI

Ufikapo mjini Mwanza; kama umeshukia kituo cha mabasi cha Nyamhongolo panda daladala ziendazo Nyashishi, Usagara na ushukie Nyegezi Kona. Kisha panda daladala, bajaji ziendazo Sweya/Luchelele – Mzunguko (Malimbe -SAUT) na ushukie kituo cha Nganza kanisani.

Au kwa atakayeshukia kitua cha mabasi cha Nyegezi (Nyegezi Bus Terminal) apande daladala ziendazo mjini na ashuke Nyegezi Kona. Kisha panda daladala ziendazo Sweya/Luchelele/ – Mzunguko (Malimbe) na ushukie kituo cha Nganza Kanisani.

Au atakayekuja na usafiri wa meli, uliza kilipo kituo cha Sweya/Luchelele (Malimbe/ SAUT) kipo barabara ya Kenyatta maarufu kwa jina la Stand ya Igombe. Kisha panda daladala ziendazo Sweya/Luchelele – Mzunguko (Malimbe) na ushukie kituo cha Nganza Kanisani

Au atakayekuja na usafiri wa anga apande daladala zinazotekea Airport kwenda Nyashishi/Usagara na ashukie Nyegezi Kona. Kisha panda daladala ziendazo Sweya/Luchelele – Mzunguko (Malimbe-SAUT) na ashukie kituo cha Nganza Kanisani Nauli ni kati ya Tsh. 700 hadi 1000

Muhula wa masomo utaanza tarehe .......................... Hivyo, mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni tarehe ........................... Mwisho wa kuripoti ni tarehe ...................... Muda wa kuripoti ni kuanzia 02:00 asubuhi – 11:00 jioni siku za kazi tu.

## 2.0 SARE ZA SHULE NA MAHITAJI YA MWANAFUNZI

### 2.1 SARE ZA SHULE

a) Sare ya shule ni sketi mbili (02) rangi ya **BLUE BAHARI** kitambaa cha suti, sketi ndefu yenye mfuko, yenye urefu wa sentimita 12 kutoka magotini na marinda 16 yaelekee upande mmoja na zipu pembeni. Kwa anayehitaji kununua shuleni zinapatikana shuleni.
b) Shati nyeupe 2 za mikono mirefu zenye kora kitambaa cha tetron au harua.

c) Hijab 2 (kijuba) iwe ni tetron/harua nyeupe ifunike kifua, ifike kwenye kifundo cha kiganja, ndefu usawa wa mikono ya shati hii ni kwa waislamu pekee.
d) Sare ya michezo kwa shule hii ni **“TRACK SUIT DARK BLUE** na **T-SHIRT** ya kijivu yenye kora nyeusi. Ziwe na nembo ya shule na kwa anayehitaji kununua shuleni zinapatikana katika duka la shule.

e) Viatu vya shule ni vyeusi **(VIWE VYA NGOZI**) vya kufunga na kamba vyenye visigino vifupi visiwe vya aina ya buti, shupapi, simpo n.k mwanafunzi aje na Raba nyeupe za michezo.
f) Soksi nyeupe na nyeusi ndefu (**stocking large**). Jozi mbili kila moja ndefu.
g) Sweta rangi ya bluu (**ROYAL BLUE** ) lenye nembo ya shule (Kwa anayehitaji kununua shuleni zinapatikana shuleni).
h) Magauni mawili ya kushindia **(SHAMBA DRESS)** ni rangi ya **“PINK”** Kwa anayehitaji kununua shuleni yanapatikana shuleni
i) Tai 02 zenye mistari ya punda milia nyeupe na blue Kwa anayehitaji kununua shuleni zinapatikana shuleni
j) Mashuka mawili blue bahari 01 na pink 01

***(N.B: KWA BAADHI YA MAHITAJI YANAYOPATIKANA SHULENI UNAWEZA KUNUNULIA SHULENI KAMA UTAPENDA)***

## 2.2. MAHITAJI BINAFSI

- Vyombo vya chakula ( sahani, bakuli, kijiko na chupa ya maji ya kunywa viwe vya mfupa. Vyombo vya plastiki haviruhusiwi.
- Vifaa vya darasani ( mathematical set, counter book quire three - kwa masomo ya sanaa na biashara yasipungue kum na masomo ya sayansi yasipungue 12, kalamu za kutosha, rula na penseli).Vilevile aje na madaftari ya kawaida 10 kwa ajili ya mazoezi ya darasani.
- Aje na taa ya solar isiwe na mwanga hafifu kwa tahadhari
- Aje na sabuni za kuogea na kufulia, taulo, kanga na kitenge pea 01, vibanio vya nguo, nguo ya kulalia na nguo za ndani za kutosha.Vikoi haviruhusiwi
- Aje na kamba za kuanikia nguo
- Aje na godoro futi 2.5 kwa 6, neti nyeupe, ndoo ndogo, foronya 2 za mto (moja blue bahari na nyingine pink) pamoja na blanketi.

## 2.3 VIFAA VYA USAFI

| DARASA | KIFAA |
|---|---|
| HGK | JEMBE LENYE MPINI 01, CHELEWA 02 |
| PGM | PANGA 01, KWANJA 01 NA CHELEWA 02 |
| PCM | MKASI 01 WA KUKATIA MAUA |
| CBG,PCB | HARD BROOM 01, HAND BRUSH 01 NA CHELEWA 02. |
| HKL,EGM,HGE | COBWEB REMOVER YA PLASTIKI 01, TOILET BRUSH NA KOPO LAKE 01 NA CHELEWA 02 |
| $EB_UAc$, $B_UA_CM$, HGL | KWANJA 01, HAND BRUSH 01 NA CHELEWA 02 |

**ANGALIZO:** Mwanafunzi alete kifaa kama ilivyo ainishwa kwa kila Tahasusi Anayosoma. Pia madarasa yanayoleta **CHELEWA IWE NDEFU KUBWA ILIYOSOKOTWA KWA WAYA**

## 2.4 VIFAA VYA MASOMO/TAALUMA

i). Graph PAD NNE kwa masomo ya Sayansi, Biashara na wale wanaosoma somo la Jiografia. GRAPH PAD MBILI atabaki nazo mwanafunzi na MBILI atakabidhi shuleni.

- Rimu 2 za karatasi (**A4 Double A tu)** )

- Vitabu vya masomo kulingana na tahasusi (Combination) husika angalia kiambatisho B

- **Dissecting kit** kwa wanafunzi wa "**biology".**

- Scientific calculator (Casio Fx 991 MS) au (Casio Fx 991 ES )orginal

## 2.5 MICHANGO INAYOTAKIWA KULIPWA NI:

| Na | Aina ya Mchango | Kiasi |
|---|---|---|
| 1. | Mchango wa Uendeshaji wa Shule | 65,000/= |
| 3. | Tahadhari | 5,000/= |
| 4. | Nembo | 5,000/= |
| 5. | Kitambulisho cha Shule | 5,000/= |
| | **Jumla** | **80,000/=** |

**Tanbihi:** Fedha yote ya michango ilipwe katika Benki ya NMB; Jina la Akaunti ni **Nganza Secondary School – School Fund, Account No. 31101100036.**

**YAFUATAYO NI YA KUZINGATIWA**

- Mzazi hakikisha unamfungulia mtoto akaunti ya benki **NMB/CRDB** kwa maswala ya kifedha, yenye uwezo wa kutoa pesa kwa **WAKAL** na **ATM**, (mwanafunzi anaweza kufunguliwa akaunti akiwa shuleni pia). Haitaruhusiwa kutuma pesa kupitia simu za walimu au mtumishi yeyote.
- Jukumu la matibabu ni la mzazi/mlezi hivyo mzazi unashauriwa kumtafutia mwanao bima ya afya akiwa nyumbani. Kwa ambaye hatakuwa na bima ya afya aje na shilingi 50,400/= kwa ajili ya kumuunga na mfuko wa bima ya afya kwa wanafunzi. Pesa hii **ISIWEKWE KWENYE AKAUNTI YA SHULE** mwanafunzi aje nayo mkononi

## 3.0. Sheria na Kanuni muhimu za Shule

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyo rekebishwa kwa Sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia yenye dhamana ya elimu na Ofisi ya waziri mkuu tawala za mikoa serikali za mitaa yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yanafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni. Mambo hayo ni pamoja na;

- Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.;

- Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule;
- Kushiriki kwa kikamilifu masomo ya asubuhi na usiku( Preparation);
- Kuwahi katika kila shughuli za shule utakazopewa;
- Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo ya kuwepo ndani na nje wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii;
- Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule;
- Kuvaa sare ya shule wakati wote kulingana na taratibu za shule.
- Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote;
- Kutunza mali za shule;
- Ni marufuku mwanafunzi kumiliki vifaa vyenye ncha kali shuleni
- Ni marufuku mwanafunzi kumiliki au kutumia dawa au vifaa tiba shuleni bila idhini ya muuguzi wa shule.
- Mwanafunzi haruhusiwi kubadili dini wala kumshawishi mwanafunzi mwenzake kubadili dini wawapo shuleni.
- Mwanafunzi haruhusiwi kujihusisha na biashara yoyote awapo shuleni
- Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawapo shuleni

- Mwanafunzi haruhusiwi kuja na, au kumiliki au kutumia simu na viambata vyake shuleni kwa namna yoyote ile, na haruhusiwi kutunza vifaa tajwa hapo juu kwa mtumishi yeyote wa shule.
- Mwanafunzi awapo shuleni atatakiwa kulala kwenye Bweni alilopangiwa na kitanda alichopangiwa. Ni marufuku mwanafunzi kulala kitanda kimoja na mwenzake au kuishi kwenye Bweni ambalo hakupangiwa. Kitanda kimoja kitatumika na mwanafunzi mmoja tu;
- Mwanafunzi ataruhusiwa kurudi nyumbani kwa ruhusa na kibali maalum toka kwa Mkuu wa Shule. (Msiba au Ugonjwa).
- Mwanafunzi haruhusiwi kuja na dawa za kienyeji
- Mwanafunzi mwenye matatizo ya afya ya kudumu aje na dawa anazotumia, zitakabidhiwa kwa muuguzi wa shule
- Mwenye matatizo ya afya kama sicklecell, Asthma au allegy inayotokana na baridi aje na pullneck nyeupe au rangi ya blue bahari

**3.1. Makosa yatakayosababisha Mwanafunzi kufukuzwa Shule ni pamoja na:**

- Wizi;
- Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro;
- Kugoma na kuhamasisha mgomo;
- Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla;
- Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yeyote yule;
- Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya dawa za kulevya;
- Uvutaji wa sigara;
- Uasherati, mahusiano ya jinsia moja au kuolewa;
- Kupata ujauzito au kutoa mimba;
- Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi;
- Kwenda kwenye nyumba za starehe na nyumba za kulala wageni;
- Kumiliki, kutumia au kukutwa na simu ya mkononi katika mazingira ya shule;
- Kudharau Bendera ya Taifa;
- Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu; na
- Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi.

**4. Viambatanisho na fomu Muhimu**

- Fomu ya uchunguzi wa Afya (Medical Examination form) ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa Hospital ya Serikali.
- Fomu ya maelezo binafsi kuhusu historia ya mwanafunzi
- Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yanayotolewa na shule,
- Picha nne za Wazazi na ndugu wa karibu wa mwanafunzi watakao wajibika wakati wote mwanafunzi awapo shuleni pamoja na namba za simu.
- Picha mbili za passport akabidhi clinic ya shule

**5. Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.**

**Tanbihi:** Mwanafunzi anapokuja kuripoti shuleni aje:-

- Kwa atakayehamia baada ya masomo kuanza aje na matokeo ya shule alikotoka

**KARIBU SANA KATIKA SHULE HII.**

Jina la Mkuu wa Shule: **Ifigenia W.Haule**
Saini ya Mkuu wa shule: .......................................
Mhuri wa Mkuu wa Shule: ...................................

**NB: Kwa siku za hivi karibuni kumekuwa na utapeli (wizi kwa njia ya mitandao). Baadhi ya wazazi wamekuwa wakitumiwa ujumbe mfupi au kupigiwa simu na watu wanaojitambulisha kama walimu na kuwafahamisha kuwa mtoto wa mzazi husika ambaye ni mwanafunzi ni mgojwa na yuko mahututi hivyo mzazi atume pesa. TAFADHALI UPATAPO UJUMBE WOWOTE KUHUSU MWANAFUNZI/MTOTO WAKO USITUME CHOCHOTE, NI VEMA UKAWASILIANA NA UONGOZI WA SHULE KUPATA UKWELI WA TAARIFA HUSIKA.**

**NGANZA SECONDARY SCHOOL**
**P.O. BOX 1252,**
**MWANZA.**

**STUDENT MEDICAL EXAMINATION FORM**

Student’s Name ............................................................... Age ...............................

Class/form V. ..........................................................................................................

Blood Examination: HB .............................................. B/S ...................................

Stool Examination: ......................................................................................

Analysis: ...........................................................................................................

UPT.....................................................................................................................

Ear .........................................................................................................................

Eye ....................................................................................................................

Chest Pain ..............................................................................................................

Allergies ...................................................................................................................

TB ..............................................................................................................................

Any Chronic Complaints note noted above e.g. Asthma, Heard Diseases, Skin Diseases, Ulcers, etc.

.......................................................................................................................

.......................................................................................................................

.......................................................................................................................

Any treatment given or recommended:-

- .......................................................................................................
- .......................................................................................................
- .......................................................................................................

Signature of Examiner ...............................................................................

Signature of Medical Officer incharge ....................................................................

Official Stamp ...........................................................................................

Date .........................................................................................................

## FOMU YA KURIPOTI SHULENI
## SHULE YA SEKONDARI NGANZA

Tarehe ya kuingia Shuleni ............................... Admission No. ...........................

Jina la Mwanafunzi ..............................................................................................

Darasa na mchepuo anoingia .................................................................................

Kabila ............................................................................

Tarehe ya kuzaliwa .............................................. Wilaya .................................

Jina la baba/mlezi ...................................................................................................

Kazi ya baba/mlezi ..................................................................................................

Namba ya simu ya baba/mlezi ...............................................................................

Mahali baba/mlezi anapoishi .................................................................................

## HISTORIA YA MWANAFUNZI

| Picha |
| --- |

Jina la Mwanafunzi ..................................................Mchepuo.....................

Dini/Dhehebu ..........................................................................................

Michezo aipendayo au hobby. ..................................................................

(a) **Taarifa za Baba**

| Picha |
| --- |

Jina la Baba…….. ......................................................(HAI/AMEFARIKI)

Dini/Dhehebu ..........................................................................................

Kazi ya baba ………………. ...................................................................

Mahali baba anaishi

Kijiji .......................................... Wilaya ................................ Anwani yake .......................... Namba yake ya Simu ....................................................

(b) **Taarifa za Mama**

| Picha |
| --- |

Jina la Mama…….... ......................................................(HAI/AMEFARIKI)

Dini/madhehebu ..........................................................................................

Kazi ya mama ……………… ...................................................................

Mahali baba anaishi

Kijiji ................................................. Wilaya .................................... Anwani yake.................................... Namba yake ya Simu ..........................................

| Picha |
| --- |

(c) **Taarifa za Mlezi anayehusika na taarifa za mwanafunzi Awapo shuleni**

Jina la Mlezi…….. ..........................................................................

Uhusiano ……………………………………………………………

Dini/Dhehebu ..................................................................................

Kazi ya Mlezi ……………........................................................................

Mahali Mlezi anakoishi:

Mtaa/Kijiji ................................................................ Wilaya .....................................
Anwani yake ...............................................................

Namba yake ya Simu ..................................................

Tatizo la kiafya la mwanafunzi (lipo/halipo) kama lipo eleza:
..........................................................................................................................
..........................................................................................................................
..........................................................................................................................
..........................................................................................................................
..........................................................................................................................
...................................................

Taja ndugu/walezi wengine wanne watakaowajibika na mwanafunzi awapo shuleni:

1. ....................................................................... simu ...................................
2. ................................................................ simu .........................................
3. ....................................................................... simu ...................................
4. ..................................................................... simu ...................................

Jina la mwanafunzi .......................................................... sahihi yake ....................

Darasa na tahasusi anayosoma ..........................................................................

## MAELEZO YAKE KUHUSU TAALUMA

Malengo yangu katika kufaulu mitihani ya masomo nitakayochukua ni:

| | MASOMO | ALAMA/GRADE |
|---|---|---|
| 1. | ........................................................... | .............................. |
| 2. | ................................................................. | ...................................... |
| 3. | ............................................................... | ...................................... |
| 4. | ..................................................................... | ...................................... |
| 5. | ..................................................................... | ...................................... |
| 6. | ..................................................................... | ...................................... |

Mikakati yangu ili kufikia malengo hayo:

i. ........................................................................................................................
ii. ........................................................................................................................
iii. ........................................................................................................................
iv. ........................................................................................................................

Nikishindwa kufikia malengo yangu nini kifanyike?

.................................................................................................................................
.................................................................................................................................
...................................................................................................................

## MWANAFUNZI KUKIRI KUZIFUATA SHERIA NA TARATIBU ZOTE ZA SHULE

Mimi ......................................................................................... wa kidato cha tano tahasusi ya ................................. nimezisoma na kuzielewa, na kuzikubali sheria, kanuni na taratibu zote za shule kama zilivyoorodheshwa hapo juu.

.............................................

**SAHIHI YA MWANAFUNZI**

**AHADI YA MZAZI**

Mimi mzazi/mlezi wa ........................................................................................ naahidi kumhimiza mtoto wangu kusoma kwa bidii, kulipa  michango yote ya shule na maelekezo mengine yatakayotolewa na shule ikiwa ni pamoja na kuhudhuria vikao vya wazazi shuleni na kufuatilia maendeleo yake ya taaluma.

Jina la mzazi/mlezi ......................................... Sahihi ya mzazi/mlezi ....................

## KIAMBATANISHO A: BEI ZA MAHITAJI YANAYOPATIKANA SHULENI

1. Track suit Dark blue pamoja yenye nembo @ 21,000/=
2. Mashati meupe mikono mirefu @ 10,000/=
3. Soksi ndefu nyeupe (Stocking large) @ 2,000/= na nyeusi ndefu @ 1,000/=
4. Sweta royal blue @ 11,000/= yenye nembo
5. Tai ya pundamilia (nyeupe na blue) @ 5,000/=
6. T- shirt ya kijivu yenye nembo ya shule @ 11,000/=
7. Daftari Quire Three @ 3,000/=
8. Ream A4 Double A @ 20,000/=
9. Godoro ft 2 ½ kwa 6

| **Aina ya Godoro** | **Bei ya Godoro** |
|---|---:|
| Superbanco | 60,000/= |
| Malaika | 35,000/= |
| Delux | 43,500/= |

10. Scientific Calculator 40,000/=
11. Mashuka 7,000/=
12. Blanketi 17,000/=
13. Chandarua nyeupe 6,000/=
14. Vyombo vya chakula 2,000/=
15. Ndoo ndogo lita kumi zenye mfuniko 3,000/= na 5,000/=
16. Vifaa vya usafi mfano: - Kwanja, 7,000/= Chelewa iliyofungwa na waya 3,000/= Jembe na mpini 10,000/=
17. Tranka 25,000/= kwa 30,000/=

## SARE ZA SHULE ZINAZOSHONWA HAPA SHULENI NA GHARAMA ZAKE

| S/N | AINA YA SARE | KIASI (TSHS) | IDADI | KIASI JUMLA |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Sketi | 22,000/= | 2 | 44,000/= |
| 2 | Gauni la kushindia | 25,000/= | 2 | 50,000/= |

## KIAMBATANISHO B: ORODHA YA VITABU

**BIOLOGY**

1. BIOLOGY FOR SECONDARY SCHOOL FORM V – TIE
2. BIOLOGICAL SCIENCE – DENNIS TAYLOR e.t al

**CHEMISTRY**

1. CHEMISTRY FOR SECONDARY SCHOOLS FORM V & VI -TIE
2. CONCEPTUAL CHEMISTRY FOR CLASS XI & XII – S. CHAND’S

**PHYSICS**

1. PHYSICS FOR SECONDARY SCHOOLS FORM V & VI – TIE
2. PRINCIPLES OF PHYSICS XI & XII– S. CHAND’S

**GEOGRAPHY**

1. PRACTICAL GEOGRAPHY FOR SECONDARY SCHOOLS FORM V & VI – TIE
2. PHYSICAL GEOGRAPHY FOR SECONDARY SCHOOLS FORM V & VI – TIE

**KISWAHILI**

1. KISWAHILI SHULE ZA SEKONDARI (LUGHA NA SARUFI) – TIE
2. FASIHI YA KISWAHILI SHULE ZA SEKONDARI (KIDATO CHA TANO MTAALA MPYA)-Mwl Maeda
3. TAHAKIKI VITABU TEULE VYA FASIHI KIDATO CHA 5 NA 6 – CHACHA S.M

**VITABU TEULE VYA KISWAHILI**

**A: RIWAYA**

1. DUNIA UWANJA WA FUJO
2. MIRATHI YA HATARI
3. WASIFU WA SITI BINTI SAAD

**B: TAMTHILIA**

1. MUKWAVA WA UHEHE
2. SHUJAA MILAMBO

3. USALITI MJINI

**C: USHAIRI**

1. FUMBO LINALOELEA
2. MALENGA WA ZIWA KUU
3. ANDAMO MSAFIRI

**ENGLISH LANGUAGE**

1. ENGLISH FOR ADVANCED SECONDARY SCHOOL (FORM FIVE & 6) - TIE

**A. NOVELS**

1. ANIMAL FARM by George Orwell - East Africa Publishers
2. CHASING THE LEOPARD FINDING THE LION by Kulie
3. WAKEMAN-LYNN - Mkuki na Nyota Publisher
4. THE OPPORTUNIST ELUTE by Nyambari Nyangwine Mbesa Books Distributors
5. THE HORIZON UNVEILED by Fellowes Mwaisela - FGD Tanzania Ltd.

**B. PLAYS**

1. THE GOVERNMENT INSPECTOR by Nikolai Gogol - East

   Africa Education Publisher

2. A TASTE OF HEAVEN by Farouk Topan - Mkuki na Nyota Publisher

**C. POETRY.**

1. SUMMONS: POEMS FROM TANZANIA by Richard S. Mabala & Et al
2. POETS OF AFRICA: Lament of the Silence & Other Poems by Jared Angira - East Africa Education Publishers

**HISTORY**

1. HISTORY FOR ADVANCED SECONDARY SCHOOLS. STUDENT’S BOOK FORM V & VI - TIE

**HISTORIA NA MAADILI YA TANZANIA**

1. HISTORIA NA MAADILI YA TANZANIA – TIE

**ACADEMIC COMMUNICATION**

1. ACADEMIC COMMUNICATION - TIE

**ADVANCED MATHEMATICS**

1. ADVANCED MATHEMATICS FORM V & VI - TIE

2. PURE MATHEMATICS 1 - L. BOSTOCK, S CHANDLER)

3. S. CHAND’S MATHEMATICS FOR CLASS XI - (H.K DASS & DR. RAMA VERMA)

4. CONCISE ADVANCED MATHS – P. L. Mayombya

**BASIC APPLIED MATHEMATICS**

1. BASIC APPLIED MATHS FOR ADVANCED LEVEL SECONDARY SCHOOLS STUDENTS’ BOOK FORM V&VI -TIE

**ECONOMICS**

1. MICROECONOMICS FIVE – TIE
2. MACROECONOMICS SIX – TIE
3. ECONOMICS I &2 - AMBROS ODHIAMBO

**ACCOUNTANCY**

1. ACCOUNTANCY FOR SECONDARY SCHOOLS FORM V & VI – TIE
2. ADVANCED ACCOUNTANCY Vol. 1 & 2 – MAHESWARI
3. SIMPLIFIED ACCOUNTING – SALEMI
4. BUSINESS ACCOUNTING Vol. 1&2 - FRANKWOOD

**BUSINESS STUDIES**

1. BUSINESS STUDIES FOR SECONDARY SCHOOLS FORM V & VI – TIE